**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Pemba*
*14 Machi, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA
## SALAMU ZA POLE

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha aliyekuwa Gavana wa nne wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dkt. Idris Rashid aliyefariki dunia leo mchana katika Hospitali ya Shifaa Pan African, Kinondoni, jijini Dar es Salaam, alikokuwa akipatiwa matibabu.

Enzi za uhai wake, Dkt. Rashid aliwahi kuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania kuanzia mwaka 1993 hadi mwaka 1998, akitoa mchango mkubwa katika kusimamia sera za fedha na kuimarisha misingi ya uthabiti wa sekta ya fedha nchini katika kipindi hicho.

Rais Dkt. Samia ameiombea roho ya Marehemu pumziko la milele, na kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa Marehemu pamoja na viongozi na wafanyakazi wa Benki Kuu ya Tanzania na Watanzania kwa ujumla.

***"Ninatoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa Marehemu Dkt. Idris Rashid. Taifa limepoteza kiongozi na mtumishi aliyetoa mchango muhimu katika ujenzi wa taasisi ya fedha na maendeleo ya uchumi wa nchi yetu,"*** amesema Rais Dkt. Samia.

Shaaban Kissu
K.n.y. Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu